

2021-0171

DAYSTAR UNIVERSITY

DAYSTAR
UNI
APP
PROG
2009

MTAALA WA KISWAHILI

MTAALA HUU UMEPENDEKEZWA KWA WANAFUNZI WA
KISWAHILI KATIKA MASOMO YA SHAHADA YA B.A (ARTS)

SILABASI HII IMEWASILISHWA KWA
COMMISSION FOR HIGHER EDUCATION

NAIROBI

JUNE 25 2009

This Proposal was approved
by the Commission for
Higher Education on
25/03/2009
[Signature]
AUTHORISED SIGNATURE

SHAHADA YA B.A. (ARTS) YA KISWAHILI

1. SABABU ZA KUANDAA MTAALA HUU

Kiswahili ni Lugha ya Taifa nchini Kenya na Tanzania. Aidha Kiswahili ni lugha inayozungumzwa katika nchi nyingi kote duniani na hasa katika nchi tatu za Afrika Mashariki. Nchini Kenya, Lugha hii ni somo la lazima katika shule za msingi na za upili. Nchini Tanzania, Kiswahili ndiyo lugha inayotumika kufundishia masomo yote katika shule za msingi. Kiswahili kinaendelea kustawi nchini Uganda na pia katika nchi za Afrika ya Kati. Umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya kimataifa unazidi kuongezeka kwa kuteuliwa kwake kuwa mojawapo kati ya lugha rasmi za Muungano wa Afrika Mashariki (EAC), Muungano wa Afrika (AU) na viungo vingine kama vile bunge la Afrika. Fauka wa hayo, Kiswahili ni mojawapo wa lugha zinazotumiwa katika shirika la Umoja wa Mataifa ambao umeanzisha huduma za tafsiri kwa Kiswahili. Isitoshe, changamoto nyingi zinazidi kutolewa na matumizi ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano katika mtandao, katika tarakilishi, katika maandishi ya Kimtandao, katika uwanja wa tafsiri na katika vyombo mbalimbali vya habari, hapa nchini na kwingineko.

Mtaala huu unanuiwa kutoa mafunzo mwafaka kwa wanafunzi ili waweze kutumia taaluma ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali na vilevile katika sekta tofauti za maendeleo ya jamii barani Afrika na duniani kwa jumla.

2. MALENGO

Kufikia mwisho wa kozi, mwanafunzi aweze:

- 2.1. Kujieleza vyema kwa kutumia stadi mwafaka za mawasiliano.
- 2.2. Kutumia nadharia zifaazo katika kuchambua lugha na fasihi ya Kiswahili kwa kuzingatia mikondo ya kitaaluma ya kisasa.
- 2.3. Kufafanua mawanda ya lugha na fasihi katika miktadha ya historia na utamaduni wa Kiafrika.
- 2.4. Kutekeleza majukumu ya kuandaa mafunzo na kuongoza katika nyadhifa mbalimbali za kijamii kwa kutumia ujuzi aliopata.
- 2.5. Kubainisha kufahamikiwa kwake vyema zaidi na mambo ya usomi kwa jumla.
- 2.6. Kubaini umuhimu wa lugha za Kiafrika hasa katika enzi ya utandawazi.
- 2.7. kushiriki masuala ibuka ikiwemo sera na upangaji wa lugha, uamilifu na utendaji kazi wake katika miktadha na mazingira mbalimbali ya mawasiliano na utoaji wa huduma na maendeleo katika jamii.

3. MAHITAJI YA KUJIUNGA NA KOZI

Pamoja na kutimiza masharti ya chuo ya kijumla, mwanafunzi anayenuia kutaalimikia somo la Kiswahili anahitaji kupata alama ya B- katika somo la Kiswahili katika mtihani wa KCSE, au "alama" 5 katika elimu ya mfumo wa awali nchini Kenya, au asilimia sitini na tano (65%) katika mifumo inayotumia tuzo za asilimia au alama A hadi E katika mfumo wa elimu wa "A".

4. TATHMINI

Jumla ya tuzo zifuatazo zitazingatiwa katika kila kozi:

| | | |
|-----------|---------------------|-------|
| Mtihani: | Asilimia sabini | (70%) |
| Mijarabu: | Asilimia thelathini | (30%) |

5. MASHARTI YA KUFUZU

Ili kufuzu na shahada ya B.A (Kiswahili) mwanafunzi anapaswa kutimiza masharti yafuatayo:

- kufanya kozi ishirini na nne (24) katika lugha.na fasihi kumi na nane zikiwa za lazima na sita za kuchagua.
- kufanya kozi ishirini za elimu ya jumla (General Education)
- kufanya kozi angalau mbili za uchaguzi huru

Ili kuhitimu mwanafunzi atahitajika awe ametimiza masaa ya kiusomi (credit hours) yasiyopungua mia moja ishirini na tisa na kujipatia jumla ya pointi **2.00** za chini kabisa kwenye kiwango cha GPA. Kozi zitafuata mpangilio ufuatao:

| | |
|---|------------|
| Masomo ya Jumla (General Education) | Masaa 51 |
| Lugha na Fasihi | Masaa 72 |
| Uchaguzi huru | Masaa 6 |
| Jumla ya Masaa ya kiusomi (credit hours) | 129 |

Taz. Saa moja la kiusomi ni sawa na maaa kumi na sita ya darasani (contact hours). Kila mwanafunzi atahitajika kusoma kwa masaa yasiyopungua efu mbili na sitini na nne (2064 contact hours) kabla ya kukubaliwa kufuzu kwa shahada ya B.A katika Kiswahili.